Kijarida Kuhusu

MIRATHI

Kimeandaliwa na:

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu

© LHRC

Septemba, 2013

Yaliyomo

SHUKURANI.....iv

UTAMBULISHO WA KITUO CHA SHERIA NA HAKI ZA BINADAMU.....iv

MAONO.....v

TAMKO LA LENGO MAHUSUSI.....vi

LENGO KUU.....vi

DIBAJI.....vii

1.0: Maana ya Mirathi.....1

1.1: Aina za Mirathi.....1

2.0: Taratibu za Kisheria Zinazohusiana na Mirathi.....1

2.1: Penye Wosia:..... 1

2.2: Pasipo na wosia..... 4

3.0: Panapokuwa na Pingamizi.....5

4.0: Mgawanyo wa Mali ya Marehemu..... 6

4.1: Sheria ya Urithi ya India ya 1865....7

4.2: Sheria ya Kiislamu.....8

4.3: Sheria ya Kimila.....9

5.0: Wajibu wa Msimamizi wa Mirathi.....10
6.0: Hitimisho.....12

SHUKURANI

Tunatoa shukurani kwa wanasheria wetu na wale wa kujitolea katika uandaaji wa vijarida hivi. Pia tunawashukuru kwa dhati wale wote walioshiriki kwenye kukirejea kijitabu hiki ili kuandaa toleo hili la tatu hususan Wakili Harold Sungusia, Wakili Fulgence Massawe, Wakili Jeremiah Mtobesya, Bw. Rodrick Maro na Bw. Evans Sichalwe, pamoja na wafanyakazi wote wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu.

UTAMBULISHO WA KITUO CHA SHERIA NA HAKI ZA BINADAMU

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu ni shirika binafsi la kujitolea na la hiari ambalo si la kisiasa wala kibiashara. Kituo kimeandikishwa na kusajiliwa kwa mujibu wa sheria za Tanzania mnamo Septemba, 1995. Kabla ya kusajiliwa kama chombo huru, Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kilikuwa ni mradi wa haki za binadamu wa Mfuko wa Kuendeleza Elimu ya Sheria Tanzania (TANLET). Makao makuu ya Kituo ni Dar es Salaam na Arusha kuna ofisi ndogo.

MAONO

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kina tamani jamii yenye haki na usawa.

TAMKO LA LENGO MAHUSUSI

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu ni shirika lisilo la kiserikali wala kibiashara linalojibidisha kukuza uwezo wa jamii ili iweze kukuza, kuendeleza na kulinda haki za binadamu na utawala bora nchini Tanzania.

LENGO KUU

Lengo kuu la Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu ni kukuza uelewa wa sheria na haki za binadamu kwa jamii kwa ujumla na hasa wale wanajamii ambao kwa sababu moja au nyingine wameachwa nyuma. Uelewa utakuzwa kwa njia ya elimu ya uraia na msaada wa sheria.

DIBAJI

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kina azma ya kusaidia jamii ya watanzania kuwa na uwezo wa kufahamu sheria za nchi pamoja na kufahamu haki zao ili kuzilinda na kuzitetea pamoja na kuheshimu haki za wengine ili hatimaye tuwe na jamii yenye utamaduni wa kuheshimu haki za binadamu pamoja na nchi inayoheshimu utawala wa sheria.

Tunafahamu kuwa kwa raia wa kawaida si rahisi kuzifahamu sheria zetu zote, na hata baadhi tu ya sheria zinazomgusa kutokana na mfumo tulio nao, ambao hautoi nafasi kwa watu wote kujua sheria. Hali hii inasababisha watu wengi kujikuta katika matatizo ya kisheria ambayo yangeweza kuepukika kama angejua sheria. Ndio maana basi Kituo kimeamua kutoa machapisho haya na mengine, kwa lengo la kutoa msaada wa kisheria kwa raia.

Huu ni usaidizi kisheria unaotoa maelezo mafupi na ya msingi ya kisheria ili kukusaidia ndugu msomaji uweze kupata ufumbuzi au maelekezo ya

tatizo linalokusibu. Ni lengo letu kuwa, katika vijitabu hivi tunatoa usaidizi wa moja kwa moja kwako wewe pale utakapokuwa na tatizo au mmoja wa ndugu au jamaa zako wanapopata matatizo ya namna hii.

Tunachokuomba ni wewe kusoma kwa makini; na pale suala lako linapokwenda mbali zaidi ya maelezo haya, basi utafute msaada wa kisheria au uende kwa mwanasheria aliye karibu na wewe ili aweze kukusaidia. Tunaamini utapata usaidizi huu kiurahisi zaidi na maelezo yaliyomo humu yatakusaidia kwa karibu. Umalizapo, tafadhali umsaidie na mwenzako kupata usaidizi huu.

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu

1.0: Maana ya Mirathi

Ni taratibu mbali mbali za kisheria zinazoongoza uangalizi, usimamizi, umiliki na hatimaye ugawaji wa mali na pengine hata kumaliza madeni ya marehemu pamoja na mazishi.

1.1 Aina za Mirathi

Kuna aina kuu mbili za mirathi:

(a) Mirathi palipo na Wosia:

Hii hutokea wakati ambapo marehemu kabla ya kufariki aliacha maandishi/matamshi au maelezo ya namna mali yake itakavyoshughulikiwa/ itakavyomilikiwa baada ya kifo chake.

(b) Mirathi pasipo Wosia:

Hii hutokea pale ambapo marehemu hakuacha Wosia, ambapo warithi halali wa marehemu hulazimika kuchagua, kupitia mahakama, msimamizi au wasimamizi wa mirathi hiyo.

2.0: Taratibu za Kisheria Zinazohusiana na Mirathi

2.1: Penye Wosia:

(i) Ndani ya siku 30 (thelathini) baada ya kifo cha marehemu, wahusika wanapaswa kusajili kifo cha marehemu kwenye ofisi

ya vizazi na vifo ambayo iko kwa mkuu wa wilaya wa kila wilaya. Kama wahusika watachelewa kusajili kifo ndani ya siku (30) wafike kwenye ofisi hiyo ya vizazi na vifo kwa maelezo. Kifo kinasajiliwa kwenye ofisi ya mkuu wa wilaya kifo kilipotokea na si wilaya yoyote. Kama kuna matatizo kuhusu wapi kifo kisajiliwe wahusika wanaweza kuwasiliana na ofisi ya kabidhi wasii mkuu (RITA);

(ii) Mara baada ya kusajiliwa kifo cha marehemu, waombaji wanaweza kufungua shauri la mirathi mahakamani, wakiambatanisha nakala ya wosia ulioachwa na marehemu na cheti cha kifo cha marehemu;

(iii) Mhusika anaweza akafungua shauri la mirathi katika mahakama ya Mwanzo, ya Wilaya, ya Hakimu Mkazi au Mahakama Kuu kufuatana na sheria itakayotumika katika usimamizi wa mali (Kimila au Kiislam), thamani ya mali, mali ya marehemu ilipo au mahali ambapo marehemu alifanya makazi yake ya kudumu kabla ya kifo chake;

(iv) Baada ya kuwasilisha maombi ya mirathi, mahakama kwa kawaida hutoa tangazo la

mirathi kwa muda wa siku 90 kwenye gazeti linalosomwa na watu wengi au katika mbao za mahakama. Lengo ni kuwawezesha wale wasioridhika na usimamizi huo kupeleka pingamizi mahakamani. Mahakama ina uwezo wa kufupisha kipindi hiki cha tangazo la siku 90, kwa kutoa tangazo la muda mfupi zaidi kwa sababu maalum;

(v) Baada ya siku 90 kuisha au muda mfupi zaidi uliowekwa na mahakama bila pingamizi kutolewa, mahakama itamthibitisha mwombaji kuwa msimamizi au mtekelezaji wa wosia wa marehemu;

(vi) Endapo muombaji ni mtekelezaji tu wa wosia wa marehemu atalazimika kutekeleza, kuendeleza taratibu za kugawa mali za marehemu kama ifuatavyo:-

- Kukusanya mali na madeni ya marehemu na pia kutambua anaowadai;
- Kutayarisha taarifa ya awali ya maelezo/ufafanuzi wa mali zote na madeni ya marehemu (inventory);
- Mtekelezaji wa wosia atagawa mali kwa mujibu wa wosia;

- Kutoa taarifa ndani ya miezi 6 ya ukamilishwaji wa zoezi la ugawaji wa mali za marehemu mahakamani na mahakama kujiridhisha kama zoezi hilo limeendeshwa sawa;
- Mahakama kufunga jalada la mirathi kama zoezi la ugawaji limeendeshwa sawa na kukamilika.

2.2: Pasipo na wosia

(i) Utaratibu wa usajili wa kifo ni kama ilivyo kwenye utaratibu wa mirathi palipo na wosia;

(ii) Msimamizi au wasimamizi wa mirathi huteuliwa au huchaguliwa na kikao cha wanandugu au ukoo;

(iii) Mbali na cheti cha kifo cha marehemu, maombi ya usimamizi wa mirathi yanatakiwa kuambatanishwa na nakala ya muhtasari wa kikao cha wanandugu cha kumchagua msimamizi wa mirathi;

(iv) Taratibu za tangazo la siku 90 au muda mfupi, chini ya hapo, ni sawa na zile zinazotumika pale palipo na wosia;

(v) Taratibu za ukusanywaji wa mali na madeni ya marehemu pamoja na uandaaji wa taarifa ya awali ya maelezo ya mali za marehemu na madeni, zinafanana na zile zilizoelezwa kwenye mirathi palipo na wosia;

(vi) Msimamizi wa mirathi atagawa mali ya marehemu kwa warithi halali na kwa mujibu wa sheria husika yaani inayotumika kwenye mirathi hiyo;

(vii) Kutoa au kupelekea taarifa ya ugawaji wa mali za marehemu mahakamani kwa madhumuni ya kufunga jalada. (Ndani ya kipindi cha miezi 6).

3.0: Panapokuwa na Pingamizi

Ndani ya kipindi cha siku 90 au pungufu (chini ya hapo) cha tangazo la mirathi kwenye mahakama yoyote, asiyeridhika na kuthibitishwa kwa mtekelezaji wosia ama kuteuliwa kwa msimamizi wa mirathi, mtu huyo anaweza kupeleka pingamizi lake mahakamani. Mara baada ya mahakama kusikiliza pingamizi hilo inaweza kumchukulia mpingaji kama mdai (objector). Hata baada ya kuisha kwa muda wa siku 90 au muda pungufu ya hapo uliowekwa na mahakama

na msimamizi kuteuliwa kama kulikuwa na kughushi au udanganyifu kuhusiana na usimamizi, basi maombi yanaweza kupelekwa mahakamani kutaka msimamizi aondolewe na usimamizi wake kutenguliwa.

IKUMBUKWE:

Kutopeleka taarifa ya kukamilika kwa usimamizi wa mirathi ni kosa la jinai, hivyo msimamizi wa mirathi ni lazima atimize majukumu yake.

4.0: Mgawanyo wa Mali ya Marehemu

Pale palipo na wosia mara nyingi mgawanyo wa mali ya marehemu hufanywa kwa kuzingatia wosia. Ugumu hujitokeza pale pasipo na wosia ambapo ugawaji wa mali hutegemea sheria mbali mbali kutegemeana na wahusika.

Hapa nchini kwetu Tanzania sheria zifuatazo, kwa kiwango kikubwa huhusika kwa namna moja au nyingine na mambo ya ugawaji wa mali au urithishwaji wa mali ya marehemu.

4.1: Sheria ya Urithi ya India ya 1865

Hii inatumika pale ambapo itaonekana kwamba marehemu alikuwa hafuati sheria za Kiislamu wala taratibu za Kimila.

Mgawanyo wa mali kwa mujibu wa sheria ya urithi ya India:

- Kama marehemu ameacha mjane na watoto mjane atapata 1/3 na watoto 2/3 ya mali yote ya marehemu.
- Na kama marehemu hakuacha watoto, mjane atapata ½ na ½ nyingine hugawanywa sawa sawa kati ya wazazi, kaka, na dada za marehemu.

Zingatia:

Kwa mujibu wa sheria hiyo watoto wa nje ya ndoa hawana haki ya kurithi isipokuwa tu kama kuna wosia na katika wosia huo wamerithishwa mali. Pia watoto wa nje ya ndoa wanaweza kurithi kama waliwahi kuhalalishwa na marehemu wakati wa uhai wake.

4.2: Sheria ya Kiislamu

Hii hutumika kwa wafuasi wa dini ya Kiislamu.

Mgawanyo wa mali ya marehemu kwa mujibu wa sheria ya Kiislamu:

- Warithi wakuu katika sheria ya Kiislamu huwa ni mke au wake, baba, mama na watoto.
- Watoto wa kiume hustahili kupata mara mbili zaidi ya watoto wa kike.
- Wajane (wale wa marehemu) wasiozidi wanne hupata 1/8 ya mali ya marehemu kama marehemu kaacha watoto.
- ¼ ya mali ya marehemu kama marehemu hakuacha watoto.
- Baba na mama hupata 1/6 kama marehemu aliacha watoto.

Zingatia:

Mtoto aliyezaliwa nje ya ndoa hana haki ya kurithi isipokuwa kama kuna wosia.

Pia kwa mujibu wa sheria ya Kiislamu muislamu haruhusiwi kuwosia mali yake yote anaweza kuwosia 1/3 tu ya mali yake, na 2/3 ni lazima igawanywe kwa warithi wake halali kufuatana na sheria ya Kiislamu.

4.3: Sheria ya Kimila

Hii hutumika pale ambapo marehemu aliishi kwa kufuata mila na desturi za kabila lake. Sheria ya kimila itatumika pale tu wahusika wa mirathi hiyo wanatoka katika kabila moja na si vinginevyo.

Mgawanyo wa mali ya marehemu kwa mujibu wa sheria za kimila:

- Hizi zimo katika kanuni za urithi (Tangazo la Serikali Na. 436, la mwaka 1963);
- Kwa mujibu wa sheria hizi kama marehemu ameacha watoto wa kiume na wa kike hao ndio warithi pekee wa mali ya baba yao;
- Kama marehemu hakuacha watoto mali yake itarithiwa na baba, mama, kaka, dada, wajomba na shangazi zake;
- Mtoto wa kiume wa nyumba kubwa hupata sehemu kubwa ya mali akifuatiwa na watoto wengine wa kiume, na mwisho watoto wa kike wa nyumba yoyote ile hupata kiasi kidogo zaidi;
- Kwa mujibu wa sheria hii wajane hawajapewa haki ya kurithi, mjane mwenye watoto sheria inampa haki ya kuishi na kutegemea watoto wake ambao watarithi mali ya marehemu mume wake.

Zingatia:

Watoto wa nje ya ndoa hawaruhusiwi kurithi chochote isipokuwa kama walihalalishwa kufuatana na mila za kabila husika.

Mali ya marehemu kwa lengo la mirathi inahusisha mali za marehemu na siyo vinginevyo.

Mjane ambaye hana mtoto/watoto atabaki katika nyumba ya marehemu na kuitumia wakati wa uhai wake, ambapo baada ya kifo chake hugawiwa kwa warithi halali wa marehemu mume wake.

5.0: Wajibu wa Msimamizi wa Mirathi

1. Ndani ya miezi 6 baada ya kuteuliwa kuwa msimamizi wa mirathi anawajibika kutoa orodha na kiasi cha mali alizoacha marehemu, fedha taslimu, madeni pamoja na idadi ya warithi halali wa marehemu anaotegemea kuwagawia mali za marehemu;
2. Kukusanya kwa uaminifu mali za marehemu;
3. Kuorodhesha madeni yaliyoachwa na marehemu pamoja na kuyalipa madeni hayo toka kwenye mali alizoacha marehemu;

4. Kulipa gharama za mazishi na gharama za kuendesha mirathi toka kwenye mali za marehemu;

5. Kugawa mali za marehemu kwa warithi halali kama marehemu atakuwa ameacha wosia msimamizi wa mirathi atagawa kufuatana na wosia alioandika marehemu na kama hakuna wosia atagawa kulingana na sheria inayotumika kwenye mirathi: kama ni sheria ya kiislamu, kimila, au serikali (yaani sheria ya mirathi ya India 1865);

6. Kushitaki ambapo marehemu angeshitaki ili kudai haki zake au kujibu mashitaka ya madai pale ambapo kutakuwepo na madai dhidi ya marehemu;

7. Kusikiliza maelekezo yanayotolewa na mahakama kuhusiana na mirathi anayoendesha;

8. Kutoa taarifa mahakamani inayoeleza aliyoendesha mirathi na kugawa mali kwa warithi wa marehemu na hatimaye mirathi kufungwa.

6.0: Hitimisho

Ni muhimu kuzingatia kwamba msimamizi wa mirathi ni mtu anayechukua nafasi ya marehemu kisheria na mali zote za marehemu zinakuwa chini ya uangalizi wake lakini haziwi zake binafsi. Msimamizi wa mirathi si mrithi wa mali za marehemu anaweza kurithi pale ambapo yeye, licha ya kuwa msimamizi wa mirathi ya marehemu, ni mrithi halali wa marehemu kama vile ni mtoto wa marehemu.

Pia warithi wa marehemu wana haki kisheria kufungua shauri la madai dhidi ya msimamizi wa mirathi kama msimamizi wa mirathi atashindwa kutimiza wajibu wake, kufuja au kuiba mali ya marehemu nakuwakosesha haki warithi halali.

Kama utapata shida zaidi usisite kufika katika Vituo vyetu vya Msaada wa Sheria kwa maelezo zaidi.